**SAYANSI ASILIA**

Kwa upande wa sayansi asilia, Tume imekuwa ikijengea uwezo wananchi katika ngazi mbalimbali kukabiliana na mabadiliko ya tabia nchi.



**SAYANSI JAMII**

Katika miaka mitatu ya uongozi wa Rais Dk. Samia, sekta ya sayansi jamii imetekeleza shughuli zifuatazo Januari mwaka 2022, wilayani Masasi, ushiriki wa wadau katika kuimarisha mipango ya UNESCO – kupambana dhidi ya manyanyaso ya kijinsia kwa wasichana kupitia sherehe za unyago.



# TUME YA TAIFA YA UNESCO

## MJI MKONGWE WA ZANZIBAR UNAENDELEA KUHIFADHIWA

# MAFANIKIO

tume ya taifa UNESCO miaka mitatu ya Rais Dk. Samia madarakani





## MAFANIKIO TUME YA TAIFA YA UNESCO KATIKA KIPINDI CHA MIAKA MITATU YA RAIS DK. SAMIA MADARAKANI

KATIKA kusaidia maendeleo kwenye sekta ya elimu, utamaduni, masuala ya vijana na urithi wa mali kale, juhudi za kuhifadhi mji Mkongwe na utekelezaji wa jitihada za kukabili mabadiliko ya tabia nchi, Tume ya Taifa UNESCO imepata mafanikio kupitia utekelezaji wa shughuli za sekta zake tano.

Sekta hizo ni Elimu, Sayansi Asilia, Sayansi Jamii, Utamaduni na Sekta ya Habari na Mawasiliano ambapo shughuli hizo kwa pamoja zimeainishwa ifuatavyo;



**SEKTA YA ELIMU**

Mafanikio ya Tume kupitia Sekta ya Elimu ambapo Tume ya Taifa ya UNESCO imeyafikia kupitia utekelezaji wa shughuli mbalimbali.

Tume imefanikiwa kuhamasisha elimu msingi kwa watoto wa kike kwenye jamii zilizoathiriwa na utamaduni wa ndoa za umri mdogo.

Kazi hiyo imefanyika Masasi Mtwara mwezi Machi mwaka 2023 ambapo Tume ya Taifa ya UNESCO na wadau wa elimu ya unyago wamefanya mapitio ya pamoja juu ya maudhui ya elimu.

MIAKA 3 YA RAIS DK. SAMIA

unesco

# Mafanikio tume ya taifa ya UNESCO katika kipindi cha miaka mitatu ya Rais Dk. Samia madarakani

KATIKA kusaidia maendeleo kwenye sekta ya elimu, utamaduni, masuala ya vijana na urithi wa mali kale, juhudi za kuhifadhi mji Mkongwe na utekelezaji wa jitihada za kukabili mabadiliko ya tabia nchi, Tume ya Taifa UNESCO imepata mafanikio kupitia utekelezaji wa shughuli za sekta zake tano.

Sekta hizo ni Elimu, Sayansi Asilia, Sayansi Jamii, Utamaduni na Sekta ya Habari na Mawasiliano ambapo shughuli hizo kwa pamoja zimeainishwa ifuatavyo;

## SEKTA YA ELIMU

Mafanikio ya Tume kupitia Sekta ya Elimu ambapo Tume ya Taifa ya UNESCO imeyafikia kupitia utekelezaji wa shughuli mbalimbali.

Tume imefanikiwa kuhamasisha elimu msingi kwa watoto wa kike kwenye jamii zilizoathiriwa na utamaduni wa ndoa za umri mdogo.

Kazi hiyo imefanyika Masasi Mtwara mwezi Machi mwaka 2023 ambapo Tume ya Taifa ya UNESCO na wadau wa elimu ya unyago wamefanya mapitio ya pamoja juu ya maudhui ya elimu inayotolewa na namna inavyotolewa.

Ushirikishwaji huo umesaidia kuondoa mafunzo kinzani yanayoathiri upatikanaji elimu kwa watoto wa kike.

Aidha, wadau wa unyago wamepata muongozo wa pamoja katika utekelezaji wa majukumu yao ndani ya jamii.

Pia, tume ilifanikiwa kuhamasisha walimu wakujitolea kupunguza tatizo la upungufu wa walimu kisiwani Mafia mwezi Agosti mwaka 2022.

Kwa kuzingatia hali ya ufaulu duni iliyojitokeza kabla ya shughuli husika ya kuhamasisha walimu tarajali kutoka vyuo vya umma na vya binafsi kufanya mazoezi kwa vitendo kisiwani humo, vilevile kuhusisha walimu wanaosubiri ajira kufanya majitoleo yakufundisha ili kupunguza ukali wa uhaba wa walimu maeneo yenye changamoto ya miundombinu ambayo siyo rafiki kwa walimu wengi kustahimili.

Tume imefanikiwa kuhamasisha na kusaidia wanataaluma nchini kujiungana mafunzo nchini China na Poland kwa mwaka 2022-2023 kwa muda mfupi na mrefu kwa lengo la kupata mafunzo ya ziada na ujuzi kwenye eneo la utafiti.

Mafunzo haya yanaratibiwa na Tume ya Taifa ya UNESCO kwa mamlaka iliyokasimiwa na UNESCO Duniani.




*Wawakilishi wa Tume ya Taifa ya UNESCO – sekta ya Elimu pamoja na walimu wa kituo cha Elimu mbadala Wingwi Pemba*

**MWAKA 2023**

**Tume imefanikiwa kuwajengea uwezo walimu wa vituo vya elimu mbadala vya Wingwi na Rahaleo Zanzibar mwezi Oktoba mwaka 2023 katika utolewaji wa mafunzo wezeshi kiuchumi na kijamii kwa wananchi waliokosa fursa ya elimu kwenye mfumo rasmi.**

Tume imefanikiwa kuwajengea uwezo walimu wa vituo vya elimu mbadala vya Wingwi na Rahaleo Zanzibar mwezi Oktoba mwaka 2023 katika utolewaji wa mafunzo wezeshi kiuchumi na kijamii kwa wananchi waliokosa fursa ya elimu kwenye mfumo rasmi.

Aidha, Tume ya Taifa ya UNESCO imefanikiwa kuwezesha wadau wa elimu nchini kupitia vyuo vikuu mwezi Agostl mwaka 2023 kufanya tathmini ya mtazamo mpya wa utolewaji wa elimu, hivyo kutoa mapendekezo muhimu katika kusaidia taasisi zenye mamlaka ya elimu ili kuboresha utolewaji wa elimu nchini.

Kazi hiyo ilifanyika kwa kuhusisha wataalamu bobezi kutoka Chuo Kikuu Huria (OUT), DUCE, Kampala, Wizara ya Elimu na Taasisi ya Elimu nchini (TET).

Vilevile, Tume imewezesha nchi kujiunga na jukwaa la Dunia ya Kijani (Green world) kupitia divisheni ya UNESCO yenye dhamana ya mapambano ya mabadilko tabia nchi duniani.

Lakini pia, tume ili ratibu ushiriki wa nchi kwenye mkutano wa COP28 kuanzia mwezi Novemba 30 hadi Desemba 13 ambapo nchi wanachama kupitia wadau wa elimu wanahusika katika utelelezaji wa nguzo nne za kujaniisha dunia (4 PILLARS OF GREENING THE WORLD).

Katika kuratibu uwakilishi wa nchi, Tume ilifanikiwa kuandaa risala ya mkuu wa nchi na Waziri wa Elimu kwenye mkutano huo COP 28 UAE

Wawakilishi wa Tume ya Taifa ya UNESCO – sekta ya Elimu pamoja na walimu wa kituo cha Elimu mbadala Wingwi Pemba

## SAYANSI ASILIA

Kwa upande wa sayansi asilia, Tume imekuwa ikijengea uwezo wananchi katika ngazi mbalimbali kukabiliana na mabadiliko ya tabia nchi.




*Wawakilishi wa Tume ya Taifa ya UNESCO- sekta ya Sayansi Asilia katika kuhamaisha matumizi ya Sayansi kwa Maendeleo Endelevu. j*

MIAKA 3 YA RAIS DK. SAMIA

unesco

# Miaka mitatu ya Rais Dk. Samia madarakani



*Wawakilishi wa Tume ya Taifa ya UNESCO – Sekta ya Utamaduni katika kuratibu zoezi la uhifadhi wa michoro ya miamba Kondoa*



*Picha ya Pamoja ya Washiriki wa Mafunzo Zanzibar*

Katika kutekeleza hilo, tume kwa kushirikiana na wadau imeendesha mafunzo ya kutumia akili bandia kujikinga dhidi ya majanga na kukabiliana na baadhi ya matokeo ya majanga hayo

Aidha, tume ya taifa ya UNESCO imeshirikiana na wadau mbalimbali kuanzisha na kuendeleza hifadhi haina Biospheres ambapo pamoja na uhifadhi, mafunzo ya namna ya kutunza maliasili na kukabiliana na mabadiliko ya tabia nchi hutolewa kwa vitendo na kuhamasisha ili kujali sayari yetu.

Tume imeanzisha hifadhi hai maeneo tengevu oevu (Wetlands) ili kulinda vyanzo vya maji, uzalishaji wa samaki, biodiversity na kujenga majukwaa ya uzalishaji endelevu usioharibu mazingira.

Lakini pia, tume imekuwa mstari wa mbele kuhamasisha matumizi ya sayansi katika maendeleo endelevu, matumizi sahihi ya nishati na kutoa fursa kwa vyanzo vipya vya uzalishaji ambavyo vinaondokana na uharibifu wa mazingira mfano hifadhi hai ya Usambara Mashariki (East Usambara Biosphere Reserve)

Wawakilishi wa Tume ya Taifa ya UNESCO - Sekta ya Sayansi Asilia wakiwa mkoani GEITA kuhamasisha uwekaji miundombinu ya maji pamoja na uhifadhi na utunzaji wa raslimali maji

### SAYANSI JAMII

Katika miaka mitatu ya uongozi wa Rais Dk. Samia, sekta ya sayansi jamii imetekeleza shughuli zifuatazo

Januari mwaka 2022, wilayani Masasi, ushiriki wa wadau katika kuimarisha mipango ya UNESCO – kupambana dhidi ya manyanyaso ya kijinsia kwa wasichana kupitia sherehe za unyago.

Februari 2022, Mapambano dhidi ya unyanyasaji wa kimwili na kukatili wa kijinsia katika Mkoa wa Tabora.

Februari mwaka 2022, mkoani Tabora utekelezaji wa mdahalo wa maadili ya kibaiolojia (Bioethics) katika Chuo cha Afya na Sayansi Shirikishi Tabora.

Agosti mwaka 2022 ilifanyika programu za kujenga ufahamu na uelewa kuhusu umuhimu wa kutekeleza Lengo la Maendeleo Endelevu namba 5 (Strategic Development Goal 5) inayohusu usawa wa kijinsia

Oktoba mwaka 2022 wadau Zanzibar walijengewa uwezo wadau wa michezo na vijana kuhusu mkataba wa UNESCO dhidi ya matumizi ya dawa haramu za kuongeza nguvu katika michezo

Decemba mwaka 2022 mafunzo yalitolewa kwa wadau kuhusu Usimamizi wa Mabadiliko ya Kijamii (MOST), maabara za siku zijazo za kusoma na kuandika na sera shirikishi.





*Wawakilishi wa Tume ya Taifa ya UNESCO - Sekta ya Sayansi Asilia wakiwa mkoani GEITA kufanikisha uwekezaji miundombinu ya maji pamoja na uhifadhi na utunzaji wa raslimali maji.*

## MRADI WA MAJI KATOMA WAMTUA MAMA NDOO KICHWANI

**Tume ya Taifa ya UNESCO imewezesha ujenzi wa mradi wa maji katika Kijiji cha Katoma mkoani Geita ambapo sasa wananchi wa kijiji hicho wanatumia maji safi na salama, hivyo kuondokana na maradhi ya mlipuko.**

**Matokeo ya mradi huo ni baada ya Tume ya Taifa ya UNESCO kwa kushirikiana na Taasisi ya Taifa ya Utafiti wa Magonjwa ya Binadamu (NIMR) walibaini changamoto ya uhaba wa maji kwa wakazi wa kijiji hicho ambapo utafiti ulifanyika kubaini kama kuna eneo lenye maji ya kutosha kuweza kuhudumia watu.**

**Baada ya eneo hilo kupatikana, Tume ya Taifa UNESCO imewezesha shughuli za uchimbaji kisima kisha uwekaji wa pampu.**

**Kwa sasa wananchi wa Kijiji cha Katoma wanapata huduma ya maji safi na salama kupitia vituo vinne vya kuchotea maji vilivyowekwa kijijini hapo.**

**Awali, kabla ya mradi huo wananchi hao walikuwa wakitumia sh. 1000 kununua ndoo sita za maji kiasi ambacho kilikuwa kikubwa lakini sasa wanatumia sh. 1000 kununua ndoo 20 za maji safi.**



*Tume ya Taifa ya UNESCO ya Jamhuri ya Mungano wa Tanzania yachangia kumtua mama ndoo kata ya katoma wilaya ya Geita*

MIAKA 3 YA RAIS DK. SAMIA

unesco

# UTAMADUNI NA URITHI WA DUNIA

Kadhalika, Februali 2023 warsha za uongozi na ushirikishwaji wa kiraia kwa vijana na Jukwaa la vijana la UNESCO, iliendeshwa.

Septemba mwaka 2023 elimu ilitolewa kwa jamii kuhusu madhara ya mimba za ututoni na namna ya kukabiliana na changamoto hiyo Wilaya ya Shinyanga vijijini.

Novemba mwaka 2023, kushiriki katika jukwaa la UNESCO la vijana kujadili namna ya kukabiliana na athari za mabadiliko ya hali ya hewa huko Paris nchini Ufaransa.



*Wawakilishi wa Tume ya Taifa ya UNESCO pamoja na wanafunzi wasichana katika kuhamasisha Elimu juu ya ndoa za ututoni mkoani Shinyanga mwaka 2023.*

## MAFANIKIO YALIYOPATIKANA

Mafanikio yaliyopatikana ni kuongezeka uelewa wa jamii kuachana na mila zinazokandamiza utu wa mwanamke. (utu, haki na thamani ya wanawake vimeongezeka).

Mbinu bora na mikakati ya kupambana na unyanyasaji wa kimwili na kijinsia, zimewekwa.

Changamoto za kimaadili katika utoaji wa huduma za afya zimeibuliwa na kuwekewa mikakati ya kukabiliananazo.

Usawa wa kijinsia na ushiriki sawa kati ya wanawake na wanaume katika shughuli za kijamii umeongezeka.

Muingiliano watamaduni kama zana maalumu kwa ujenzi wa amani na mshikamano wa wanajamii umeongezeka.

Jamii imejengewa uelewa juu ya sababu za mimba za ututoni, madhara na namna ya kukabiliana nazo.

Tume ya Taifa ya UNESCO ilifanikiwa kupeleka mshiriki katika jukwaa la UNESCO la vijana nchini Ufaransa kujadili namna ya kukabiliana na athari za mabadiliko ya hali ya hewa.

Kupitia kijana huyo vijana nchini watanufaika na mafunzo hayo ambayo yapo kwenye maandalizi yatakayowajengea uwezo wa kufanya shughuli za kiuchumi pasipo kuharibu hali ya hewa na mazingira kwa ujumla.

Wawakilishi wa Tume ya Taifa ya UNESCO pamoja na wanafunzi wasichana katika kuhamasisha Elimu mkoani Shinyanga mwaka 2023

## UTAMADUNI NA URITHI WA DUNIA

Tume imeratibu mchakato wa kutafuta fedha na kufanikiwa kupata wafadhili na kuweza kufanya ukarabati wa majengo na magofu ya kale kadhaa ya urithi wa dunia.

Mradi huu umetekelezwa ili kuhifadhi michoro ya miamba Kondoa mkoani Dodoma, kudhibiti maji ya

> **UNESCO**
>
> **Tume ya Taifa ya UNESCO ilishiriki kikao kilichoitishwa na Wizara ya Utamaduni, Sanaa na Michezo kilichofanyika tarehe 10 Julai 2023 kuhusu urejeshwaji wa masalia na vifaa vya kiutamaduni vilivyochukuliwa wakati na baada ya ukoloni.**
>
> .

Bahari yasiendelee kumomonyoa magofu-kale ya Kilwa Kisiwani na Songomnara yaliyopo Kilwa mkoani Lindi, kuhimili jengo la maajabu la (Beit el ajaib) na kuimarisha elimu ya urithi katika mji Mkongwe wa Zanzibar.

Tume ya Taifa UNESCO imefanikiwa kusimamia shughuli za uendeshaji na usimamizi wa maeneo ya hifadhi ambayo ni ya kiutamaduni na kiasili kwa maendeleo endelevu jambo hilo limesaidia kuongeza vivutio vya utalii.

Mfano, Tume imesimamia uendelezaji na utunzaji wa Hifadhi ya Taifa ya Ngorongoro kupitia utoaji wa elimu shawishi ya uhamaji wa hiyari kwa wananchi waliokuwa wanachangia uharibifu wa ekolojia ya hifadhi kuhamia Kijiji cha Msomera, wilayani Handeni mkoani Tanga.

Tume imefanikiwa kuratibu mchakato wa kukiwezesha Kiswahili (lugha ya Kiswahili) kuwa miongoni mwa lugha za Kimataifa.

Jambo hilo limefanyika Julai Mosi mwaka 2022 mjini Paris nchini Ufaransa ambapo wajumbe wawili toka Tume ya Taifa UNESCO waliiwakilisha Tume.

Tume ilifanikiwa kuandaa kikao cha kujadili mpango wa ujenzi wa bwawa katika hifadhi ya Selou.

Aidha, Tume ilifanikiwa kuandaa muongozo wa kiutafiti kuonesha kuwa mradi huo hautakuwa na madhara ya kiikolojia kwa hifadhi hiyo ambayo ni miongoni mwa hifadhi zilizoko kwenye orodha za urithi wa dunia.

Tume ya Taifa ya UNESCO ilishiriki kikao kilichoitishwa na Wizara ya Utamaduni, Sanaa na Michezo kilichofanyika tarehe 10 Julai 2023 kuhusu urejeshwaji wa masalia na vifaa vya kiutamaduni vilivyochukuliwa wakati na baada ya ukoloni.

Kikao kilibaini kuwa kumekuwepo na juhudi za Wizara na Taasisi za Serikali pamoja na Asasi za Kiraia na watu binafsi wanaofuatilia masalia au vifaa vya kiutamaduni vinavyohusiana na koo zao. Hali hiyo ya kukosekana uratibu unafifisha juhudi za kupatikana kwa masalia au vifaa hivyo.

Kwa kuwa kuna taarifa kwamba Wizara ya Maliasili na Utalii inafanya juhudi kama hizo, kikao kilimuomba Katibu Mkuu wa Wizara ya Utamaduni, Sanaa na Michezo, kuwasiliana na Katibu Mkuu wa Wizara ya Maliasili kutafuta namna bora ya kuratibu jambo hilo kitu ambacho kitasaidia kwa upande mwingine.

Wawakilishi wa Tume ya Taifa ya UNESCO – Sekta ya utamaduni katika kuratibu zoezila uhifadhi wa michoro ya miamba Kondoa

## JUHUDI ZA TUME YA TAIFA YA UNESCO KWA KUSHIRIKIANA NA SERIKALI KUHAKIKISHA MJI MKONGWE WA ZANZIBAR UNAENDELEA KUHIFADHIWA

Katika eneo la Mji Mkongwe wa Zanzibar, semina za kuhamasisha jamii zinazoishi katika eneo la urithi wa dunia zilifanyika katika mji mkongwe wa Unguja Zanzibar, ambazo zilihusiana na uhifadhi na utunzaji wa mazingira ndani na nje ya eneo la urithi.

Tume ya Taifa ya UNESCO iliratibu warsha ya mradi wa Revitalising Stone town of Zanzibar Social Economic Development 25-27 Julai 2023 ambapo aliyekuwa Waziri wa Utalii na Urithi wa Zanzibar, Mhe. Simai Mohammed Said, alifanya uzinduzi huo.

Mradi huu unafadhiliwa na Serikali ya Oman na unalengo la kuhifadhi utamaduni pamoja na kuimarisha uhifadhi na usimamizi wa miji ya kihistoria ikiwemo Mji Mkongwe ambao ni Urithi wa Dunia.

MIAKA 3 YA RAIS DK. SAMIA

# SEKTA YA HABARI NA MAWASILIANO

### MAENEO AMBAYO SEKTA YA UTAMADUNI IMEJIKITA KUHAKIKISHA JAMII INAPATA UELEWA KUHUSU ATHARI ZA MABADILIKO YA TABIA YA NCHI

Maeneo ambayo sekta ya utamaduni imejikita kwa lengo la kuhakikisha jamii inapata uelewa kuhusu athari za mabadiliko ya tabia nchi ni maeneo yote ya urithi wa Dunia yanayopatikana nchini Tanzania

Maeneo hayo ni Ngorongoro World Heritage Site, Mount Kilimanjaro World Heritage Site, Selous Game Reserve World Heritage Sites, Serengeti National Park, Ruins of Kilwa Kisiwani and Ruins of SongoMnara World Heritage Site, Kondoa Rock Art, Stone Town of Zanzibar World Heritage Site

### HATUA ZA KUCHUKUA KUKABILIANA NA HALI HIYO

Tume imesimamia uendelezaji na utunzaji wa hifadhi ya Taifa ya Ngorongoro kupitia utaoaji wa elimu shawishi ya uhamaji wa hiari kwa wanachi waliokuwa wanachangia uharibifu wa ikolojia ya hifadhi kuhamia Kijiji cha Msomera wilayani Handeni mkoani Tanga.

Wananchi wanaoishi maeneo ya KINAPA walipatiwa elimu ya mazingira na kutathimini urithi wa utamaduni kwa maendeleo endelevu, pia kulifanyika tathimini ya mahitaji kutambua fursa za ajira kwa vijana na kukuza ujuzi kwa vijana na wanawake katika eneo hilo la urithi wa Dunia wa hifadhi ya Taifa ya Kilimanjaro.

### SEKTA YA HABARI NA MAWASILIANO

Katika sekta hii shughulizi zilizofanyika ni kutoa mafunzo kwa wadau mbalimbali wahabari Unguja na Pemba juu ya nafasi ya vyombo vya habari katika kuchangia utawala wa haki na sheria katika jamii.

**SEPTEMBA 2023**

**Kupitia miradi ya ushirikishwaji (Participation Programme – PP) ya UNESCO, Tume kwa kushirikianana Idara ya Habari Maelezo Zanzibar iliandaa mafunzo kwa Maofisa Habari na Mawasiliano wa Umma na Binafsi yaliyofanyika kuanzia Septemba 2023 Unguja na Pemba.**

Mafunzo hayo yalilenga katika kuhamasisha na kujenga tabia ya kuheshimu utawala wa haki na sheria katika jamii uliojikita kwenye misingi ya kupata habari za uhakika kutoka vyanzo sahihi kwa wakati kwa ajili ya kufanya maamuzi sahihi.

Jumla ya washiriki 23 wakiwemo wanahabari, wanafunzi wanaosomea taaluma ya habari, wanaharakati, wanasheria na wawakilishi wa serikali kutoka Unguja na Pemba walijengewa uwezo katika kuimarisha utawala wa haki na sheria katika jamii.

Tume kupitia Sekta ya Habari na Mawasiliano ilishiriki katika mikutano iliyoendeshwa kimtandao kama ifuatavyo:

Mjadala wa Kamati za Dunia za Kumbukumbu za Kikanda kati ya Asia na Afrika juu ya usimamizi, michakato ya kuanzisha na kuorodhesha rejista za kikanda zitakazosaidia uanzishwaji wa Rejista ya Kumbukumbu za Dunia (Memory of the World) ya Afrika katika siku zijazo.

Majadiliano juu ya Mpango wa Utekelezaji wa Umoja wa Mataifa kuhusu Usalama wa Wanahabari (UNPA) barani Afrika.

Mkutano wa Tume za Kitaifa za UNESCO juu ya utekelezaji wa sheria katika nyanja ya mawasiliano na habari.

Mkutano huu ulijikita katika mambo makubwa matatu ambayo ni matumizi ya lugha nyingi katika muktadha mmoja, njia za pamoja za upatikanaji wa taarifa kimtandao, urithiwa nyaraka katika mfumo wa kidijiti.

Tume imeratibu utekelezaji wa mapendekezo ya UNESCO yaliyopitishwa katika Mkutano Mkuu wa Mwaka 2015 kuhusu usalama na utunzaji wa Hati za Urithi wa Nyaraka Kidigitali.

Ufuatiliaji huo ulifanyika katika Ofisi ya Kumbukumbu na Nyaraka ya Taifa na Taasisi ya Kumbukumbu na Nyaraka Zanzibar kwa lengo la kuwezesha nyaraka hizo kuhifadhi kwa muda mrefu na kupatikana kwa urahisi.

Kupitia miradi ya ushirikishwaji (Participation Programme – PP) ya UNESCO, Tume kwa kushirikianana Idara ya Habari Maelezo Zanzibar iliandaa mafunzo kwa Maofisa Habari na Mawasiliano wa Umma na Binafsi yaliyofanyika kuanzia Septemba 2023 Unguja na Pemba.

Mafunzo hayo yalilenga kuimarisha uwezo wa Maofisa Habari wa Umma, Binafsi na wafanyakazi wa vyombo vya habari katika kutoa taarifa za serikali kwa wananchi kwa uwazi pamoja na kufundisha umma kutumia fursa za teknolojia za sasa katika upatikanaji wa habari.

Jumla ya Maofisa Habari wa Umma, Binafsi na wafanyakazi wa vyombo vya habari 20 kutoka Unguja na 20 kutoka Pemba walishiriki.




*Picha ya Pamoja ya Washiriki wa Mafunzo Zanzibar*